JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

# UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA – TCRA KATIKA KUADHIMISHA SIKU YA USALAMA MTANDAONI MWAKA 2020 *(SAFER INTERNET DAY 2020)*

Siku ya tarehe 11 Februari, 2020 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeadhimisha Siku ya Usalama Mtandaoni (*Safer Internet Day*) nchini katika ukumbi wa maktaba kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Maadhimisho ya Siku ya Usalama Mtandaoni ni mpango wa kimataifa wenye lengo la kuhamasisha matumizi bora na salama ya mtandao wa intaneti.

Siku hii ambayo huadhimishwa wiki ya pili ya mwezi Februari kila mwaka, huunganisha mamilioni ya watu ulimwenguni kwa nia ya kuhamasisha matumizi sahihi ya mtandao ili kuimarisha usalama wa anga la mtandao dhidi ya athari za kiusalama kwa kutoa elimu ya vionjo mbalimbali vinavyohamasisha matumizi bora ya mtandao kwa kuzingatia kanuni na miongozo ya kiusalama.

Katika zama hizi za kidijitali ambapo utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kila siku katika jamii hutegemea Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), mtandao ni nyenzo muhimu ya kuiwezesha jamii kushiriki ipasavyo kwenye uchumi wa kidijitali (digital economy) na hivyo kujipatia maendeleo ya kiuchumi. Mtandao umetoa fursa mbalimbali za kiuchumi kama vile kufanya biashara za kibenki kwa njia ya simu, kutafuta masoko kwa njia ya mitandao ya kijamii na hivyo kuiwezesha jamii ya Watanzania husuan vijana kujipatia kipato.

Miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia maendeleo makubwa ya sekta ya mawasiliano nchini. Jamii kubwa ya Watanzania mijini na vijijini imefikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu na mtandao wa intaneti. Huduma ya mtandao kwa kiasi kikubwa imekuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mtandao kwa asili yake ya muunganiko na kutokuwa na mipaka, umepelekea nchi zote ulimwenguni kukumbana na athari za kiusalama. Hivyo, ni muhimu kwa wadau ulimwenguni kote kushirikiana ipasavyo katika kukabiliana na changamoto za kiusalama ili kuujenga mtandao ulio bora na salama kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni ***"pamoja kwa mtandao bora"*. **Hivyo basi jamii nzima haina budi kushirikiana ili kuhakikisha anga la mtandao linakuwa salama kwa watu wa rika zote.

Kwa muktadha huo, kila mdau wa mawasiliano ana jukumu la kutekeleza ili kuimarisha usalama wa mtandao dhidi ya matukio hatarishi ya kiusalama kwa kufanya yafuatayo: -

1. ***Watoto na vijana*** – mnawajibika kuufanya mtandao kuwa salama kwa kuwa waadilifu mnapokuwa mnatumia mitandao, kulinda heshima zenu na za wenzenu walioko mtandaoni.

   Mtumie teknolojia hii kwa fursa chanya kama vile kujielimisha, kujadili mambo ya msingi na yenye staha, kufanya ushirikika wenye mlengo chanya, kujiburudisha kwa kuzingatia miongozo na kanuni mbalimbali za kijamii, tamaduni zetu na kanuni za kiusalama zilizopo;

2. ***Wazazi na Walezi*** – tuwawezeshe na kuwasaidia vijana/watoto wetu kutumia teknolojia ipasavyo kwa sisi mwenyewe kuwa mfano bora, mfano kwa heshima, tahadhari na kuzingatia kanuni za usalama (*security best practises*).

3. ***Waalimu na wakufunzi*** – kujenga mtandao bora kwa kuwaandaa wanafunzi na elimu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kwa kuandaa vipindi vya kuelimisha zaidi matumizi ya TEHAMA na kutengeneza maudhui yatakayotumika kuelimisha umma kwani ukielimisha mtoto mmoja hapa ataelimisha kumi afikapo nyumbani au anapokuwepo kwenye jamii inayomzunguka.

4. ***Watoa huduma ya mtandao (Internet Service Providers)*** – Kuimarisha ulinzi wa miundombinu ya mtandao dhidi ya hatari na kiusalama (cyber-threats) na hivyo kutoa huduma bora ya mtandao zitakazojenga na sio kubomoa maadili ya jamii. Tuwe na vipindi vya kuelimisha umma sambamba na kutoa huduma hii ya intaneti.

5. ***Watoa huduma za maudhui mtandaoni (Online Content Service Providers)*** – kutengeneza maudhui bora na salama kwa kuzingatia kanuni za maudhui matandaoni i.e ***The Electronic and Postal Communications (Online Content) Regulations, 2018*** yanayokidhi mahitaji ya jamii yetu.

6. ***Watoa maamuzi –*** Kutunga sera, sheria na kanuni zitakazochangia kukuwa kwa TEHAMA hapa nchini kwani ni dhahiri kuwa hatuwezi kuepuka teknolojia hii kama tunataka kuendana na maendeleo ya hivi sasa ambapo kitu ni dijitali.

7. ***Kila mtumiaji wa mtandao*** anawajibika kutumia mtandao kwa usahihi na kwa kuzingatia taratibu, kanuni, sheria na sera za kitaifa na kimataifa.

Pamoja na majukumu hayo ya kimakundi, sote tunawajibika pia **kuripoti matukio ya usalama mtandaoni** kwa **"TZ-CERT"** kwa ajili ya ushauri na msaada wa kiufundi kwani imeanzishwa kutoa huduma kwa wananchi. Mnakaribishwa sana kutembelea TCRA Makao Makuu hapo mtapata fursa ya kujua zaidi TZ-CERT au kuitembelea mtandaoni kwa kupitia tovuti yao ya www.tzcert.go.tz.

Ni kwa kutambua umuhimu wa mtandao katika kuongeza tija na ufanisi na mchango kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali yetu imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha usalama wa mtandao na watumiaji wake. Jitihada hizo ni pamoja na kuanzishwa kwa kituo cha kitaifa cha mwitikio wa kukabiliana na majanga ya kompyuta kijulikanacho kama ***Tanzania Computer Emergency Response Team*** kwa ufupisho "**TZ-CERT**". Kituo hiki kiliundwa mwaka 2010 ndani ya muundo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Baadhi ya majukumu ya TZ-CERT ni:-

i. Kutoa elimu na kuhamasisha matumizi bora na salama ya mtandao na mifumo ya TEHAMA;

ii. Kufanya tathmini ya mashambulizi ya kiusalama kwenye miundombinu muhimu ya TEHAMA nchini ili kubaini madhaifu yaliyoko na kuchukua hatua stahiki. Huduma hii hutolewa bila ya malipo yoyote;

iii. Kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA kwenye eneo la usalama mtandao ili kuongeza ujuzi na weledi wa kukabiliana na matukio ya kiusalama;

iv. Kutoa angalizo na ushauri kwa wadau wake na jamii kwa ujumla juu ya hatari za kiusalama na hatua stahiki za kuchukua kuepuka athari za kiusalama.

Mwisho, kwa kushirikiana pamoja tutaweza kuujenga mtandao bora na salama kwa manufaa yetu binafsi na Taifa kwa ujumla.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**